JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI
SHULE YA SEKONDARI MWAMLAPA

S.L.P 228,

BARIADI - SIMIYU.

TAR_____

KUMB. MSS/BDC/JI/2020/2

NDG. MZAZI/MLEZI WA _____

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAMLAPA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2020.</u>

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari MWAMLAPA mwaka wa masomo 2021. Shule hii ni ya kutwa na mchanganyiko (Wasichana na Wavulana). Hongera sana.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Hivyo,mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** kwa ajili ya usajili na kuanza masomo. **MWISHO WA KURIPOTI NI TAREHE 22/01/2021, Mwanafunzi akichelewa au asipofika kuripoti kuanza masomo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtoto na mzazi au mlezi**. Ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha kuwa mwanafunzi anawahi shuleni bila kukosa au kuchelewa baada ya kukamilisha mahitaji na taratibu zote zilizoelekezwa katika barua hii.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo wilaya ya Bariadi Vijijini, tarafa ya Mhango kata ya Kasoli katika Kijiji cha Mwamlapa. Umbali kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Bariadi ni Km. 75.

MASOMO YANAYOFUNDISHWA SHULENI:

Atakapo kuwa hapa shuleni atapaswa kusoma masomo tisa 9 ambayo ni **CIVICS, HISTORY, GEOGRAPHY, ENGLISH LANGUAGE, KISWAHILI, PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY, BASIC MATHEMATICS**. Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kingereza isipokuwa somo la kiswahili. Lugha ya mawasiliano shuleni ni kingereza tu.

MAHITAJI

A. NDANI YA DARASA

1. Daftari kubwa za kutosha
2. Mathematical set 1
3. Kalamu za wino na penseli za kutosha
4. Mfuko wa madaftari (school bag)
5. Kamusi ya kingereza – kingereza {dictionary}

B. SARE YA SHULE

1. **WAVULANA**: Awe na shati mbili nyeupe mikono mifupi, tai mbili dark blue na damu ya mzee, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufungwa kwa kamba, soksi nyeusi jozi mbili, suruali moja rangi ya Light blue (Bluu Bahari) na nyingine rangi ya Damu ya mzee (suruali iwe pana siyo chupa (model) , iwe na mifuko mitatu miwili mbele na mmoja nyuma) na sweta rangi ya bluu Bahari.
2. **WASICHANA**: Awe na shati mbili mikono mifupi na tai rangi ya Light blue na damu ya mzee, viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi, soksi nyeupe jozi mbili, sketi mbili moja rangi ya Light bluu (Blue Bahari), nyingine ya damu ya mzee kitambaa kizito, sketi iwe ndefu kuvuka magoti kwenda chini, sweta rangi ya bluu.

NB: MAVAZI YASIYO YA HESHIMA HAYATAKIWI

Sare ya shule itavaliwa wakati wote mwanafunzi awapo shuleni, darasani, shughuli zote za kishule na wakati wa safari nje ya shule. Katika michezo kila mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare ya michezo

3. **VIFAA VYA USAFI**: Mwanafunzi anatakiwa kuja na ufagio wa nje (chelewa), ndoo ndogo ya lita 10 na jembe moja kwa ajili ya shughuli za usafi na kazi za mikono(shamba la shule).

ANGALIZO

- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa viatu vya ghorofa (visigino virefu)
- Ni marufuku kwa mwanafuzi kuvaa nguo zisizo rasmi shuleni
- Ni marufuku mwanafunzi kuvaa suruali mlegezo(kata K) na ukibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako
- Kila mwanafunzi anapaswa kuwa safi, kufanya usafi kikamilifu katika eneola shule alilopangiwa kila siku
- Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu kanuni, taratibu na sheria za shule. Hivyo, lazima awe na nidhamu ya hhali ya juu.

C. MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi atatambulishwa mipaka ya shule na kuifahamu. Hivyo,

i. Ni marufuku mwanafunzi kuwa nje ya eneo la shule katika muda anaotakiwa kuwepo shuleni bila ruhusa maalumu.
ii. Ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo hata kama sio muda wa shule:-
    - Nyumba za kulala wageni(Guest house/Lodge)
    - Vilabu vya pombe(Bar)
    - Nyumba za walimu na Ofisi bila kibali
    - Kumbi za starehe

Pamoja na barua hii, nakufungashia fomu mbalimbali ambazo ni lazima zijazwe kikamilifu kabla ya kusajiliwa na msajili wa wanafunzi hapa shuleni. Fomu hizo ni pamoja na sheria za shule, taarifa binafsi za mwanafunzi na vipimo vya daktari (medical examination form) na uthibitisho wa mzazi/mlezi.

KARIBU SANA MWAMLAPA SEKONDARI

_____

ADILI D. MWAIPOPO
MKUU WA SHULE
0757391563/0782659496

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

3.1: Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandaishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wa shule, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa kama mwanafunzi katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule na za Umma

3.2. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule**;

(a) Wizi (b) Uasherati na ushoga (c) Ubakaji (d) Kupiga au kupigana
(e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, n.k
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma (g) Kudharau Bendera ya Taifa (h) Kupata mimba au kumpa mtu mimba (i) Kuoa au kuolewa (j) Kutoa mimba (k) Kuwa na simu ya mkononi
(l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi

Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi;

Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

NB: **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……
ADILI D. MWAIPOPO
MKUU WA SHULE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE,TECHNOLOGY AND VOCATION TRAINING

MWAMLAPA SEKONDARI SCHOOL,

S.L.P 228,
BARIADI.
DATE……..

THE MEDICAL OFFICER,
……,
P.O.BOX ……
BARIADI.

RE: FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examine the under mentioned boy/girl as his/her fitness for studies at this school.(This form should be completed by a Government Medical Officer).

Students full name: ----------
Blood test ----------
Stool Examination: ----------
T.S.test: ----------
Asthma: - ----------
Eye disorder: ----------
Nose disorder: ----------
Skin disorder: ----------
Anaemia : ----------
Chest: - ----------
Operation: ----------
Serious Accidents: ----------
Any other infections disease: ----------
Pregnancy: ----------

ADDITIONAL INFORMATION (eg.physical defects or impairments)
Infections chronic of Family disease etc:

I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE STUDIES AS INDICATED ABOVE.

Signature: ----------
Designation: ----------
Station: - ----------

Date: -